MWONGOZO KAMILI WA NDOA YA KIISLAMU

UCHUMBA, NDOA, TALAKA NA KUNYONYESHA

SEHEMU YA PILI

IMEANDALIWA NA

ABUU ZAKARIYYAA, YAHYA HASSAN ALHANBALY

UTANGULIZI

بِسۡمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحۡمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ

Sifa Njema Zote ni stahiki ya Allah ambaye ameumba Mbingu na Ardhi na vilivyomo ndani yake na baina yake. Sala na salamu zimuendee Mtume Muhammad ﷺ, Ahli zake, Maswahaba wake na waliowafuatia kwa wema.

Katika Makala hii, nitagusia hukumu zinazofungamana na posa na uchumba katika Uislamu. Miongoni mwa nukta nitakazozigusia ni:-

1. Maana ya posa
2. Kuchagua mwenza
3. Masharti yanaozingatiwa katika kumposa mwanamke
4. Kumtazama mchumba
5. Kuvunja uchumba
6. Makosa katika uchumba

MAANA YA POSA

Amesema Sheikh Muhammad bin Swaalih Al-U'thaymin[1]

والخِطبة بكسر الخاء هي طلب التزوج من المرأة، قَالَ تَعَالَى: ﴿وَلَا جُنَاحَ عَلَيۡكُمۡ فِيمَا عَرَّضۡتُم بِهِۦ مِنۡ خِطۡبَةِ ٱلنِّسَآءِ﴾ البقرة [235]

Na 'Khitw-ba' (posa) kwa 'kasra' ya 'khaa' ni kuitaka ndoa kutoka kwa mwanamke. Amesema Allah Mtukufu "Na si vibaya kwenu katika kuwapelekea posa kwa ishara tu wanawake waliomo ndani ya eda" (Al-baqara 235)

KUCHAGUA MCHUMBA

- Vigezo anavyotakiwa mwanaume kuangalia wakati wa kuchagua mke

1. Mwanamke mwema

Mwanamke mwema Allah ﷻ amemtaja katika Qur-an kwa kusema:

﴿فَٱلصَّٰلِحَٰتُ قَٰنِتَٰتٌ حَٰفِظَٰتٞ لِّلۡغَيۡبِ بِمَا حَفِظَ ٱللَّهُۚ﴾ النساء [34]

[1] Ash-sharhul-mumtii' Juzuu 5 Uk. 754

Wanawake Wema ni watiifu, wenye kuhifadhi tupu zao na siri za waume zao wakati wa kutokuwepo kwao, kwa kuwa Allah ameamrisha wajihifadhi (An-nisaai 34)

Na katika Sunna za Mtume Muhammad ﷺ kuna muongozo wa kuchagua mke mwema

عَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رضي الله عنه، عَنِ النَّبِيِّ صلى الله عليه وسلم قَالَ: (تُنْكَحُ الْمَرْأَةُ لِأَرْبَعٍ: لِمَالِهَا وَلِحَسَبِهَا وَجَمَالِهَا وَلِدِينِهَا، فَاظْفَرْ بِذَاتِ الدِّينِ تَرِبَتْ يَدَاكَ)

Kutoka kwa Abuu Hurayra - Allah amridhie amesema: Amesema Nabii ﷺ "Huolewa Mwanamke kwa mambo manne: kwa mali yake, na kwa nasabu yake, na kwa uzuri wake, na kwa dini yake. Mpate mwenye dini, mikono yako itagusa mchanga- kwa majuto endapo usipompata mwenye dini"[1]

Hadithi hii watu wengi wanaifahamu ki makosa. Wanaona kuwa Mtume ﷺ amehimiza sifa hizo nne: mali, cheo, nasabu, na dini. Usahihi Mtume ﷺ ameelezea uhalisia wa watu wanapokwenda kuchagua mke, huwa wanatazama vigezo gani, ila yeye akahimiza kigezo kimoja cha dini, na kuwa atakayeangalia vigezo vingine na hakutazama kigezo cha dini basi atajuta kwa hilo.

2. Mwenye mapenzi na kizazi kingi

Amesema Mjumbe wa Allah ﷺ

(تَزَوَّجُوا الْوَدُودَ الْوَلُودَ، إِنِّي مُكَاثِرٌ الْأَنْبِيَاءَ يَوْمَ الْقِيَامَةِ)

"Oeni wanawake wenye mapenzi, wenye kuzaa. Kwa hakika mimi ni mwenye kujifakhari kwa Manabii kwa wingi wenu Siku ya Qiyama"[2]

Mwanamke mwenye mapenzi huonekana kupitia familia yake na ukoo wake. Kuna maeneo wanawake wao husifika kwa kuwa na mapenzi ya dhati kwa waume zao, na kuna sehemu wanawake wao husifika kwa kutokuwa na mapenzi na kutokuwa waaminifu katika ndoa zao. Vilevile; mwanamke mwenye kuzaa sana huonekana kupitia ndugu zake wa kike - mama yake, dada zake, shangazi zake n.k.

Kutokana na mitandao ya kijamii, leo hii mwanamke hutengenezewa fikra ya kuwa hakuna mapenzi kama mwanaume hana pesa. Kwahyo mapenzi yao ni katika pesa za mwanaume. Hili limepelekea madhara makubwa sana katika jamii. Kuna wanawake wamewauwa waume zao ili wabakie na mali, kuna wanaume wamewafanya wanawake ni chombo cha starehe kwa kuwa wanajua wanawake hao hawana mapenzi kwao, ni

[1] Sahihul-Bukhary, Hadithi na. 4802
[2] Musnad Ahmad, Hadithi na. 12613

kama mtu ananunua starehe kwake. Ikawa mahusiano ya kimapenzi ya sasa ni hatari mno sababu hayajengwi kwa mapenzi na huruma.

Wazazi, walezi na watu wenye kutengeneza mambo, hawanabudi kuirejesha jamii katika asili yake kwa kutumia nafasi ya kimalezi kuulekeza umma na kuubainishia ya kuwa, mwanamke kwa asili ana mapenzi ya dhati yasiyofungamana na kitu cha mtu kamavile mali, cheo cha mtu n.k. Ndio maana utasikia habari za watu wa kale kuwa, mwanamke fulani alimkataa mwanaume fulani, japo ana mali, wadhifa, na kwenda kuolewa na mwanaume masikini asiye na hadhi kabisa.

3. Awe ametoka katika mazingira mazuri ya malezi

Mwanaadamu ni mtoto wa mazingira. Mazingira ambayo anayokulia ndio hutengeneza utu wake na hulka yake. Hivyo mwanaume anatakiwa aangalie sehemu anapochukua mke. Iwe ni sehemu ambayo husifika kwa malezi bora ya watoto wa kike. Kwa hilo, Mtume wa Allah ﷺ aliwasifia Wanawake wa Kikurayshi kwa kusema

(نِسَاءُ قُرَيْشٍ خَيْرُ نِسَاءٍ رَكِبْنَ الْإِبِلَ، أَحْنَاهُ عَلَى طِفْلٍ، وَأَرْعَاهُ عَلَى زَوْجٍ فِي ذَاتِ يَدِهِ).

"Wanawake wa Kikurayshi ni bora ya wanawake waliopanda ngamia, ni wenye huruma sana kwa watoto, na ni wenye kumchunga zaidi mume kwa kilichopo katika mkono wake – wanatumia vizuri mali za waume zao, sio wabadhilifu".[1]

Sifa hizo ambazo Mjumbe wa Allah ﷺ amewasifia Wanawake wa Kikurayshi, ni sifa zitokanazo na malezi na ada ya watu wao. Hivyo; ni juu ya mwanaume kutazama eneo analokwenda kuoa na kujua sifa za wanawake wake kabla ya kuoa.

4. Hupendelewa awe mwanamwali

Mwanamke Bikra au mwanamwali ni yule ambaye kizinda chake hakijavunjwa kwa kutokuingiliwa na mwanaume[2]. Na pia hutumika kwa mwanamke ambaye bado hajaolewa. Na pia anaweza kukusudiwa mwanamke ambaye amezaa mara moja. Amesema Ibnu Faaris – Allah amrehemu

قال الخليل: والبِكْرُ من النِّساء التى لم تُمَسَسْ قطُّ. قال أبو عبيدٍ: إذا وَلَدتِ المرأةُ واحداً فهى بِكْرٌ أيضاً

Amesema Al-khaliil: Na bikra katika wanawake ni ambaye kamwe hajawahi kuingiliwa. Amesema Abuu U'bayd: Mwanamke akizaa mara moja basi naye ni bikra vilevile.[3]

[1] Sahihul-Bukhary, hadithi na. 3251
[2] Kamusi Kuu ya Kiswahili, uk. 75
[3] Mu'ujamu Maqayiis Al-lughah, Juzuu 1 Uk. 289

Lakini kuna wakati maslahi yanapaikana zaidi kwa kumuoa mwanamke mjane. Hivyo atashauriwa aoe mwanamke mjane. Kama ilivyokuja katika Kisa cha Jaabir – Allah amridhie, alipoambiwa na Mjumbe wa Allah ﷺ

(هَلْ تَزَوَّجْتَ بِكْرًا أَمْ ثَيِّبًا). فَقُلْتُ: تَزَوَّجْتُ ثَيِّبًا، فَقَالَ: (هَلَّا تَزَوَّجْتَ بِكْرًا تُلَاعِبُهَا وَتُلَاعِبُكَ). قُلْتُ: يَا رَسُولَ اللَّهِ، تُوُفِّيَ وَالِدِي، أَوِ اسْتُشْهِدَ، وَلِي أَخَوَاتٌ صِغَارٌ، فَكَرِهْتُ أَنْ أَتَزَوَّجَ مِثْلَهُنَّ فَلَا تُؤَدِّبُهُنَّ وَلَا تَقُومُ عَلَيْهِنَّ، فَتَزَوَّجْتُ ثَيِّبًا لِتَقُومَ عَلَيْهِنَّ وَتُؤَدِّبَهُنَّ

“Je umeoa bikra au mjane?” (Akasema Jaabir) nikasema: Nimeoa mjane. Akasema - Mtume ﷺ “Basi si ungeoa bikra, ukacheza naye na akacheza na wewe!”. Nikasema: Ewe Mjumbe wa Allah! Amefishwa baba yangu, au amekufa shahidi, na mimi nina dada wadogo, sikupenda kuoa mfano wao ambaye hawezi kuwaadabisha na kuwasimamia. Hivyo; nikaoa mjane ili awasimamie na kuwaadabisha[1]

Katika hadithi hii, tunapata faida ya kupendelewa kuoa mwanamke bikra. Na mwanamke mjane huolewa kwa maslahi, kamavile: kuwa ni mwenye kusimamia malezi ya watoto walio chini ya mume, au kuwalea mayatima walio chini ya mwanamke huyo, kumuhifadhi na kumnusuru kutokana na zinaa n.k.

Ama miongoni mwa faida za kupendelewa kuoa mwanamke bikra ni:Kupata kustarehe naye kwa kucheza naye, kwani kwa mwanamke bikra ambaye mara nyingi huwa na umri mdogo, hupendelea michezo, hili jambo humpa mume starehe, utulivu na maliwazo kutokana na mazonge ya kimaisha. Na pia ametaja Sheikh Ibnu U’thaymiin – Allah amrehemu faida nyingine kwa kusema:

فالبكر أفضل؛ لأنها لم تطمح إلى رجال سابقين، ولم يتعلق قلبها بأحد قبله، ولأن أول من يباشرها من الرجال هذا الرجل، فتتعلق به أكثر

Basi bikra ni bora zaidi (kumuoa), kwasababu anakuwa hajawa na pupa kwa wanaume waliotangulia. Na moyo wake haujafungamana na yeyote hapo kabla. Na ya kwamba, wa mwanzo kumuingilia katika wanaume ni huyu mwanaume (mumewe), basi atajifungaminisha naye zaidi[2]

Kwa kauli hii, tunaona umuhimu wa kumuoa mwanamke bikra kuwa ni miongoni mwa sababu za mwanamke kuwa muaminifu katika ndoa yake. Baadhi ya ndoa zimekuwa na changamoto ya wanawake kutoka nje ya ndoa zao kwasababu, mwanamke anakuwa ameolewa ila bado anaendeleza mahusioano na mwanaume aliyekuwa naye mwanzo. Ila kwa mwanamke bikra anakuwa hajui mapenzi isipokuwa ni ya mwanaume huyo, hivyo inakuwa ni vigumu kushawishika na kutoka katika ndoa yake.

[1] Sahihul-Bukhary, hadithi na. 2805
[2] Ash-sharhul Mumtii’ Juzuu 5 Uk. 747

- Vigezo anavyotakiwa mwanamke kuangalia wakati wa kuchagua mume

1. **Awe na tabia njema na dini**
   Amesema Mjumbe wa Allah ﷺ:

   إذا خَطَبَ إِلَيْكُم من تَرْضَوْنَ دِينَهُ وخُلُقَهُ، فزَوِّجُوهُ، إِلَّا تَفْعلُوا، تكُنْ فِتنةٌ في الأرضِ، وفَسَادٌ عَرِيضٌ

   "Pindi atakapoposa kwenu mnayemridhia dini yake na tabia yake, basi muozesheni. Endapo msipomuozesha, kutapatikana fitna katika ardhi na ufisadi mwingi[1]

2. **Awe ametoka katika mazingira mazuri ya malezi**
   Kama tulivyoonesha katika sifa ya kuchagua mke, awe ametokea katika mazingira mazuri ya malezi, sababu malezi yake ndio humfanya kuwa ni mtu wa namna gani. Vivyo hivyo mwanamke atazame sehemu ambapo aliyekuja kuposa amelelewa na kukulia. Amesema Mjumbe wa Allah ﷺ:

   النَّاسُ مَعَادِنُ، خِيَارُهُمْ فِي الْجَاهِلِيَّةِ خِيَارُهُمْ فِي الْإِسْلَامِ، إِذَا فَقُهُوا

   Watu wanatofautiana asili. Mbora wao katika Ujahili ndio mbora wao katika Uislamu, basi litambueni (hilo)[2]

3. **Asiwe tasa**
   Ukitazama wakati tunazungumzia sifa za mke wa kuoa, katika sifa na. 2, Hadithi tuliyoitaja inaonesha ya kuwa, Mjumbe wa Allah ﷺ atajifakharisha kwa wingi wa watu wake simu ya Qiyama. Ikiwa mwanaume hana uwezo wa kutungisha ujauzito basi haipendelewi mke kumchagua.

4. **Awe na uwezo wa kumuhudumia mke**
   Sheria ya Uislamu imeweka usimamizi wa huduma za mke kwa mwanume. Kama alivyosema Allah ﷻ:

   ﴿ ٱلرِّجَالُ قَوَّٰمُونَ عَلَى ٱلنِّسَآءِ بِمَا فَضَّلَ ٱللَّهُ بَعۡضَهُمۡ عَلَىٰ بَعۡضٖ وَبِمَآ أَنفَقُواْ مِنۡ أَمۡوَٰلِهِمۡۚ ﴾ النساء [34]

   Wanaume ni wasimamizi kwa wanawake, kwasababu ya kile Allah alichowafadhilisha baadhi yao kwa wengine na kwa kile **wanachokitoa katika mali zao** (Annisai, aya 34)

   Hivyo; mwanaume ikiwa hawezi kabisa kumhudumia mwanamke, basi mwanamke ana khiyari ya kutomchagua. Na hapa haizungumziwi mume kuwa tajiri ili mke aweze kuishi maisha ya anasa, bali uwezo wa kumpa kula yake, sehemu ya kukaa, mavazi yake na kumtibia akiugua, kwa kile kichache kinachoweza kufanya hayo. Ndio maana Mtume ﷺ aliwaozesha maswahaba ambao walikuawa hawana uwezo hata wa kumiliki pete ya chuma kama mahari ya mke.

[1] Sunanu At-tirmidhiy, hadithi na. 1109
[2] Sahihul-Bukhary, hadithi na. 3203

MASHARTI YANAOZINGATIWA KATIKA KUMPOSA MWANAMKE

Inashurutishwa katika kumposa mwanamke masharti mawili. Nayo ni:

1. **Asiwe mwanamke mwenye vizuizi vya kisheria**
   Vizuizi vya kisheria vinavyokusudiwa ni: asiwe mwanamke aliyeharamishwa kwake, na asiwe mwanamke huyo yupo katika eda. Ama kuhusu wanawake walioharamishwa kwa mwanaume, hili tutalielezea kwa kina katika makala zijazo In shaa Allah.

   Mwanamke aliye katika eda yake haifai kuposwa, sawasawa iwe ni eda ambayo mume anaweza kumrejea au asiyoweza kumrejea, au eda ya kufiwa. Ama ikiwa ni eda ya kutorejewa au ya kufiwa, basi inafaa kumposa bila kumwambia maneno yasiyoashiria moja kwa moja kuwa anahitaji kumuoa. Kamavile kusema: Mimi ni mwenye raghba kwako, ukimaliza eda yako niambie, usinikoseshee nafsi yako, hakika wewe ni mzuri n.k. Na hilo amelitaja Allah ﷻ:

   ﴿ وَلَا جُنَاحَ عَلَيۡكُمۡ فِيمَا عَرَّضۡتُم بِهِۦ مِنۡ خِطۡبَةِ ٱلنِّسَآءِ ﴾ البقرة [235]

   Wala hakuna ubaya kwenu kupeleka posa kwa ishara kwa wanawake waliomo katika eda (Al-baqarah, aya 235)

2. **Asiwe ametanguliwa na yeyote katika kuposa**
   Ikiwa kuna mtu tayari amekwisha kwenda kumposa mwanamke, basi mwingine hatakiwi kupeleka posa yake mpaka ile posa irejeshwe au mposaji wa mwanzo aache mwenyewe. Sababu kutofanya hivyo, kutapelekea bughudha, na uhasama baina yao. Amesema Mjumbe wa Allah ﷺ:

   (لَا يَخْطُبَ الرَّجُلُ عَلَى خِطْبَةِ أَخِيهِ، حَتَّى يَتْرُكَ الْخَاطِبُ قَبْلَهُ أَوْ يَأْذَنَ لَهُ الْخَاطِبُ)

   Asipose mtu juu ya posa ya ndugu yake (katika imani), mpaka mposaji kabla yake aache au ampe idhini[1]

KUMTAZAMA MCHUMBA

Ni jambo la kisheria kumtazama mwanamke unayekusudia kumposa ili uone katika mambo yenye kukuvutia kwake, mambo yatakayopelekea kumuoa mwanamke huyo. Vilevile na mwanamke amuone mwanaume anayemposa. Kufanya hivyo kutapelekea ndoa hiyo kudumu.

عَنِ الْمُغِيرَةِ بْنِ شُعْبَةَ، قَالَ: خَطَبْتُ امْرَأَةً، فَقَالَ لِي رَسُولُ اللهِ صلى الله عليه وسلم: (أَنَظَرْتَ إِلَيْهَا؟). قُلْتُ: لَا، قَالَ:(فَانْظُرْ إِلَيْهَا، فَإِنَّهُ أَحْرَى أَنْ يُؤْدَمَ بَيْنَكُمَا)

[1] Sahihul-Bukhary, hadithi na. 4848

Kutoka kwa Al-mughiirah bin Shuu'bah Amesema: Nilimposa mwanamke, Mtume wa Allah ﷺ akaniambia, "Umemtazama?", nikasema: hapana, akasema "Mtazame, basi hakika hilo hupelekea kudumishwa baina yenu"[1]

Katika kumtazama mwanamke unayekusudia kumuoa, haihitajiki idhini yake wala ya baba yake. Anasimulia Jaabir – Allah amridhie, pale Mtume alipomwambia akiweza kumtazama mwanamke anayemposa basi afanye hivyo:

فَخَطَبْتُ جَارِيَةً فَكُنْتُ أَتَخَبَّأُ لَهَا حَتَّى رَأَيْتُ مِنْهَا مَا دَعَانِي إِلَى نِكَاحِهَا فَتَزَوَّجْتُهَا

Basi nikamposa binti, nikawa najificha kwaajili yake (ili kumtazama) mpaka nilipoona kwake kinachonivutia kumuoa basi nikamuoa[2]

Si katika uchamungu mtu kutomtizama binti anayekusudia kumuoa, wala si katika uovu mtu kumtizama binti ili amuoe, na si uchamungu binti kukataa kuonekanwa kwa kigezo kuwa inavunja stara yake, maadamu muhusika ni mtu aliyekuwa na vigezo tajwa hapo juu, katika vigezo vye mume wa kufaa kuoa. Aliyeruhusu hilo ndio aliyeweka sheria ya mwanamke kuvaa stara. Na jambo hili pia lilikuwa zito kwa baadhi ya Maswahaba, ila baada ya kusikia ni ruhusa ya Mtume ﷺ, likawa halina budi isipokuwa kufanyika.

عَنِ الْمُغِيرَةِ بْنِ شُعْبَةَ، قَالَ: أَتَيْتُ النَّبِيَّ صلى الله عليه وسلم، فَذَكَرْتُ لَهُ امْرَأَةً أَخْطُبُهَا، فَقَالَ: " اذْهَبْ فَانْظُرْ إِلَيْهَا، فَإِنَّهُ أَجْدَرُ أَنْ يُؤْدَمَ بَيْنَكُمَا ". قَالَ: فَأَتَيْتُ امْرَأَةً مِنَ الْأَنْصَارِ، فَخَطَبْتُهَا إِلَى أَبَوَيْهَا، وَأَخْبَرْتُهُمَا بِقَوْلِ رَسُولِ اللهِ صلى الله عليه وسلم، فَكَأَنَّهُمَا كَرِهَا ذَلِكَ، قَالَ: فَسَمِعَتْ ذَلِكَ الْمَرْأَةُ وَهِيَ فِي خِدْرِهَا، فَقَالَتْ: إِنْ كَانَ رَسُولُ اللهِ صلى الله عليه وسلم أَمَرَكَ أَنْ تَنْظُرَ، فَانْظُرْ، وَإِلَّا فَإِنِّي أَنْشُدُكَ. كَأَنَّهَا عَظَّمَتْ ذَلِكَ عَلَيْهِ. قَالَ: فَنَظَرْتُ إِلَيْهَا: فَتَزَوَّجْتُهَا.

Kutoka kwa Al-mughiirah bin Shuu'bah amesema: Nilimuendea Nabii ﷺ nikamtajia kuhusu mwanamke niliyemposa. Akasema, "nenda kamtazame, kwani hilo linapelekea zaidi kudumishwa baina yenu". Akasema (Al-mughiirah): Nikamuendea mwanamke katika Answar, nikamposa kupitia kwa wazazi wake, na nikamwambia kauli ya Mjumbe wa Allah ﷺ, ni kana kwamba hawakuipenda (wazazi wake) kauli hiyo. Akasema (Al-mughiirah): Akalisikia hilo mwanamke akiwa katika stara yake, akasema, "Ikiwa Mjumbe wa Allah ﷺ amekuamrisha kutazama, basi tazama. Na ikiwa sio hivyo (hajakuamrisha kutazama) basi nakukumbusha". Kana kwamba mwanamke huyo akalifanya kubwa jambo hilo kwake (Al-mughiirah). Akasema (Al-mughiirah): Nikamtazama, kisa nikamuoa[3]

Amesema Ibn Qudaamah- Allah amrehemu:

ويجوز النظر إليها بإذنها، وبغير إذنها؛ لأن النبي صلى الله عليه وسلم أطلق النظر، فلا يجوز تقييده

Na inafaa kumtazama kwa idhini yake (binti), na pasi ya idhini yake. Kwasababu Nabii ametaja kutazama kwa ujumla, basi haijuzu kuufunga utazamaji[4]

---

[1] Musnad Ahmad, Hadithi na. 18154
[2] Sunanu Abii Daud, hadithi na. 2082
[3] Musnad Ahmad, Hadithi na. 18137
[4] Al-kaafy Juzuu 3 Uk. 5

Kadhalika, inafaa kurudia mara kadhaa kumtazama mchumba mpaka makusudio yapatikane, nayo ni kuona kile chenye kumvutia mposaji katika ndoa. Swali ni, je! Ni maeneo gani yanayofaa kumtazama mwanamke anayekusudiwa kuposwa?. Maeneo ambayo inafaa kumtazama mposwaji haiyajaanishwa katika hadithi, hivyo ikapelekea ikhtilafu ya wanachuoni katika kuanisha ni sehemu zipi ambazo zinafaa kuzitazama. Kuna ambao wanaona inafaa kumtazama uso na viganja vya mikono pekee, kuna wanaoona kinachofaa kutazama ni yale maeneo ambayo yamezoeleka kuonekana akiwa na maharimu zake na wanawake wengine kamavile: uso, nywele, shingo, mikono mpaka mabegani na miguu mpaka kwenye magoti, na hii ndio kauli ya kati na kati. Na Daud Adhwaahiry yeye ameona kufaa kumtazama mwili mzima!. Anasema A'lau Ad-diin Al-Mardawiy:

وعنه، له النَّظَرُ إلى ما يَظْهَرُ غالبًا؛ كالرَّقَبَةِ واليَدَين والقدَمَين. وهو المذهبُ. قال في «تَجْرِيدِ العنايَةِ»: هذا الأصحُّ.

Na kutoka kwake (Imam Ahmad), inafaa kutazama katika yale ambayo aghlabu yanayodhihiri, kama shingo, mikono miwili, na miguu. Na kauli hii ndiyo kauli ya Madhehebu (ya Imam Ahmad). Na amesema katika Tajriidul-I'naayah: Na kauli hii ni sahihi zaidi[1]

Kwahivyo, kauli ya wastani ni kufaa kumtazama mchumba katika maeneo ambayo aghlabu huonekana akiwa na maharimu zake.

Jambo la kuzingatia ni kwamba, anayepewa nafasi ya kumuona mchumba ni yule ambaye inatarajiwa kwake kumkubali huyo binti kulingana na vigezo vyake kwa anayekusudia kumuoa, na pia awe ni mtu ambaye yupo tayari kwa ndoa, ili kuwahifadhi mabinti kutokana na kutazamwa na kila mtu na kuhifadhi heshima zao. Amenukuu A'lau Ad-diin Al-Mardaawiy maneno ya Ibn Khatwiib aliposema:

قلتُ: ويتعَيَّنُ تقْيِيدُ ذلك بمَن إذا خطَبَها غلَب على ظَنِّه إجابتُه إلى نِكاحِها.

Ninasema: Na kinaainika kidhibiti cha hilo jambo (la kumtazama mchumba), ni kwa yule ambaye inadhaniwa zaidi kukubali kumuoa huyo mwanamke[2]

Ikiwa mposaji anakusudia kujua tabia za binti, basi atatafuta watu wa karibu wenye kumfahamu huyo binti, kama kaka zake, baba zake, mama zake, shangazi zake lakini lazima wawe ni watu wenye uadilifu. Wasipokuwa hivyo, ima watamchafua kwa sifa mbaya ikiwa hawapendi oelewe au watamsifia sifa njema ambazo huyo mwanamke hana ili aweze kuolewa.

Inafaa kwa mwanamke anayeposwa kujipamba kwa mapambo ya halali, kamavile:kupaka hina, kutia rangi za mdomo na kupaka wanja. Ama mapambo yanayotoa uhalisia wake, kama kufanya 'make-up' hili halifai, sababu huondosha uhalisia wa mposwaji. Na jambo hili la kujipamba limethibiti katika kisa cha Subaya'h binti Al-haarith Al-aslamiyyah-

[1] Al-Inswaaf, Juzuu 20 Uk. 31
[2] Al-Inswaaf, Juzuu 20 Uk. 30

Allah amridhie- kilichopo katika Sahihul-Bukhary, hadithi na. 3991, ambapo Subaya'h alijipamba baada ya kufiwa na mumewe Saa'd bin Khawla - Allah amridhie- na baada ya kumaliza eda yake kwa kujifungua. Na alijipamba kwaajili ya watakaokuja kumposa.

Na ikiwa mtu amekwenda kuposa na hakuridhika na aliyekwenda kumposa baada kumtazama, au mwanamke alimletea ujumbe kuwa anahitaji kuolewa naye, basi haitakikani kwake kumkatalia, bali itatosha kukaa kimya. Kufanya hivyo ni kwaajili ya kutouvunja na kuutia simanzi moyo wa mwanamke huyo. Amesema Ibn Hajar Al-a'sqalaaniy- Allah amrehemu:

لا ينبغي أن يصرح لها بالرد؛ بل يكفي السكوت

Haifai mwanaume kuweka wazi kumkataa, bali inatosha kukaa kimya[1]

KUVUNJA UCHUMBA

Ifaa kuuvunja uchumba ikiwa kuna sababu ya kisheria kamavile: Moja katika wachumba kukosa sifa ya dini na tabia[2], mwanaume kutoweza kumudu gharama za ndoa[3] n.k, lakini ikiwa mtu amevunja pasi na sababu ya kisheria, inakuwa makruhu, maana ni jambo ambalo linaambatana na kuuvunja moyo wa mwingine, kumtia simanzi na majonzi.

MAKOSA KATIKA UCHUMBA

Yafuatayo ni baadhi ya makosa ya kisheria ambayo wanayaingia wengi katika wachumba na ndugu wa kaaribu wa wachumba:

1. Mtu kwenda kuposa sehemu ilihali anajua kuwa huyo mwanamke tayari amekwishaposwa na mtu mwingine, ila anafanya hivyo sababu ana vishawishi vya mali hadhi n.k.
2. Kuweka uchumba kwa kuvishana pete za uchumba. Jambo hili si katika dini ya uislamu kwa chochote, bali ni katika desturi za Kikafiri. Uchumba wa kiislam ni kwa mposaji kwenda kwao na binti, kisha kufikisha jambo lake kwa walii wa binti. Amesema Sheikh Al-Albaniy – Allah amrehemu:

لبس بعض الرجال خاتم الذهب الذي يسمونه بـ "خاتم الخطبة" فهذا مع ما فيه من تقليد الكفار أيضا - لأن هذه العادة سرت إليهم من النصارى ففيه مخالفة صريحة لنصوص صحيحة تحرم خاتم الذهب على الرجال وعلى النساء أيضا

Kuvaa baadhi ya wanaume pete ya dhahabu, ambayo wanaiita pete ya uchumba, hili jambo pamoja na kuwa ndani yake kuna kuwaiga makafiri, kwasababu hili jambo ni katika desturi imewafikia wao (waislamu) kutoka kwa Manaswara

[1] Fat-hul-baary, Juzuu 9 Uk.175
[2] Rejaea fatwa na. 14095 na swali na. 5, fatwa na. 8445 ya Al-lajnatu Ad-daaimah
[3] Rejaea fatwa na. 13875 ya Al-lajnatu Ad-daaimah

(Wakristo)[1], vilevile ndani yake kuna kuhalifu dalili zilizo sahihi zenye kuharamisha pete ya dhahabu kwa wanaume na wanawake.[2]

Katika Maelezo ya Sheikh ameonesha kutofaa vitu viwili: Kuvaa pete ya uchumba kwa nia hiyo, na pili, kuvaa pete ya dhahabu, na akaonesha kuwa ni haramu kuvaa pete ya dhahabu kwa wanaume na wanawake. Ama kwa wanaume hakuna khilafu, khilafu ipo kwa upande wa wanawake, na kauli ya karibu ni kufaa wanawake kuvaa pete au mapambo ya dhahabu sababu ni katika ada yao kujipamba. Ama dalili ya kuharamisha pete ya dhahabu kwa wanaume;

عَنْ أَبِي أُمَامَةَ، أَنَّهُ سَمِعَ رَسُولَ اللهِ صلى الله عليه وسلم يَقُولُ: (مَنْ كَانَ يُؤْمِنُ بِاللهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ، فَلَا يَلْبَسْ حَرِيرًا، وَلَا ذَهَبًا)

Kutoka kwa Abuu Umama, kwamba alimsikia Mjumbe wa Allah – Sala na Salamu zimfikie akisema: Yeyote anayemuamini Allah na Siku ya Mwisho, basi asivae hariri wala dhahabu[3]

3. Ndugu wa kiume wa mposaji kumuona binti akiwa katika hali isiyo ya stara, au mposaji kuwa huru kumuoana mama wa binti, dada zake na maharimu wengine wakiwa wamepunguza stara.
4. Uzushi (bidaa) ya kusoma dua au Suuratul-faatihah kwa hoja ya kuweka ahadi madhubuti baina ya wachumba, au kuubariki uchumba n.k. Yote haya ni mambo ambayo hayajafundishwa na Uislam, na Allah hakubali matendo yaliyozushwa katika dini yake.

عن عَائِشَة أَنَّ رَسُولَ اللهِ صلى الله عليه وسلم قَالَ: (مَنْ عَمِلَ عَمَلًا لَيْسَ عَلَيْهِ أَمْرُنَا فَهُوَ رَدٌّ)

Kutoka kwa A'isha -Allah amridhie- kwamba Mjumbe wa Allah – sala na salamu zimfikie amesema: Yeyote atakayefanya jambo ambalo dini yatu haipo juu yake, basi jambo hilo ni lenye kurejeshwa kwake.[4]

5. Wachumba kwenda kutazama nyota, ili kuona kuwa wanaendana au la. Hili ni jambo la haramu na linapelekea katika shirki na kumkufuru Allah Mtukufu

عَنِ ابْنِ عَبَّاسٍ قَالَ: قَالَ النَّبِيُّ صلى الله عليه وسلم: (مَنِ اقْتَبَسَ عِلْمًا مِنَ النُّجُومِ، اقْتَبَسَ شُعْبَةً مِنَ السِّحْرِ، زَادَ مَا زَادَ)

Kutoka kwa Ibn Abbas amesema: Amesema Nabii – Juu yake sala na salamu: Yeyote atakayejifunza na kuwa na elimu ya unajimu, basi atakuwa amejifunza na kuwa na sehemu katika uchawi, atazidi katika uchawi muda atakaozidi kujifunza unajimu[5]

Mjumbe wa Allah – Juu yake sala na salamu ameonesha katika hadithi kuwa kujifunza na kubobea katika elimu ya unajimu ni kujifunza uchawi. Na tunajua kuwa kujifunza

---

[1] Katika jarida 'Woman' linachapishwa London tarehe 19/03/1960 Uk. 8, ameelezea Angela Talbot kuwa jambo la kuvalishana pete ya uchumba ni katika desturi ya Wakristo

[2] Aadabu Az-zifaaf Uk. 133

[3] Musnad Ahmad, Hadithi na. 22248

[4] Sahihul-Bukhary, hadithi na. 1718

[5] Sunanu Abii daud, Hadithi na. 3905

uchawi ni haramu, na kuufanyia kazi ni Ukafiri. Lakini swali, ni unajimu gani uliokatazwa?

عَنْ زَيْدِ بْنِ خَالِدٍ الْجُهَنِيِّ قَالَ: « صَلَّى بِنَا رَسُولُ اللهِ صلى الله عليه وسلم صَلَاةَ الصُّبْحِ بِالْحُدَيْبِيَةِ، فِي إِثْرِ السَّمَاءِ كَانَتْ مِنَ اللَّيْلِ، فَلَمَّا انْصَرَفَ أَقْبَلَ عَلَى النَّاسِ، فَقَالَ: هَلْ تَدْرُونَ مَاذَا قَالَ رَبُّكُمْ؟ قَالُوا: اللهُ وَرَسُولُهُ أَعْلَمُ، قَالَ: قَالَ: أَصْبَحَ مِنْ عِبَادِي مُؤْمِنٌ بِي وَكَافِرٌ، فَأَمَّا مَنْ قَالَ: مُطِرْنَا بِفَضْلِ اللهِ وَرَحْمَتِهِ، فَذَلِكَ مُؤْمِنٌ بِي كَافِرٌ بِالْكَوْكَبِ، وَأَمَّا مَنْ قَالَ: مُطِرْنَا بِنَوْءِ كَذَا وَكَذَا، فَذَلِكَ كَافِرٌ بِي مُؤْمِنٌ بِالْكَوْكَبِ »

Kutoka kwa Zayd Ibn Khaalid Al-juhaniy amesema: Alitusalisha Mjumbe wa Allah – Sala na Salamu zimfikie- Swala ya Asubuhi, Hudaybiyyah, baada ya mvua iliyokuwa usiku. Baada ya kumaliza akawaelekea watu na kusema " Je! Mnafahamu alichokisema Mola wenu Mlezi?" wakasema: Allah na Mtume wake ndio wajuzi zaidi. Akasema " Amesema (Mola wenu Mlezi): Wamepambaukiwa waja wangu wakiwa kuna wenye kuniamini na wenye kunikufuru. Ama walioniamini wamesema: Tumenyeshewa mvua kwa Fadhila za Allah na Rehema zake, basi hao ndio wenye kuniamini mimi, wenye kukufuru nyota. Na ama waliosema: Tumenyeshewa mvua kwa nyota fulani, hao wamenikufuru mimi na kuamini nyota.[1]

Amenukuu Al-dhwiim Aabaad –Allah amrehemu- kuelezea elimu ya unajimu iliyokatazwa:

قَالَ الْخَطَّابِيُّ عِلْمُ النُّجُومِ الْمَنْهِيُّ عَنْهُ هُوَ مَا يَدُلُّ عَلَيْهِ أَهْلُ التَّنْجِيمِ مِنْ عِلْمِ الْكَوَائِنِ وَالْحَوَادِثِ الَّتِي لَمْ تَقَعْ كَمَجِيءِ الْأَمْطَارِ وَتَغَيُّرِ الْأَسْعَارِ وَأَمَّا مَا يُعْلَمُ بِهِ أَوْقَاتُ الصَّلَاةِ وَجِهَةُ الْقِبْلَةِ فَغَيْرُ دَاخِلٍ فِيمَا نُهِيَ عَنْهُ انْتَهَى

Amesema Al-khatwaabiy: Elimu ya unajimu iliyokatazwa ni ile wanaoitolea ushahidi wanajimu katika elimu za ulimwengu na matukio ambayo hayajatokea, kama kuja kwa mvua, kubadilika kwa gharama za bidhaa. Ama kile kinachojulikana kwa elimu hiyo Nyakati za Swala na pande za Qibla, haiingii katika kilichokatazwa katika elimu ya unajimu.

وَفِي شَرْحِ السُّنَّةِ الْمَنْهِيُّ مِنْ عُلُومِ النُّجُومِ مَا يَدَّعِيهِ أَهْلُهَا مِنْ مَعْرِفَةِ الْحَوَادِثِ الَّتِي لَمْ تَقَعْ وَرُبَّمَا تَقَعُ فِي مُسْتَقْبَلِ الزَّمَانِ مِثْلُ إِخْبَارِهِمْ بِوَقْتِ هُبُوبِ الرِّيَاحِ وَمَجِيءِ مَاءِ الْمَطَرِ وَوُقُوعِ الثَّلْجِ وَظُهُورِ الْحَرِّ وَالْبَرْدِ وَتَغْيِيرِ الْأَسْعَارِ وَنَحْوِهَا وَيَزْعُمُونَ أَنَّهُمْ يَسْتَدْرِكُونَ مَعْرِفَتَهَا بِسَيْرِ الْكَوَاكِبِ وَاجْتِمَاعِهَا وَافْتِرَاقِهَا وَهَذَا عِلْمٌ اسْتَأْثَرَ اللَّهُ بِهِ لَا يَعْلَمُهُ أَحَدٌ غَيْرُهُ

Na katika Sharhu Sunna: Kilichokatazwa ni elimu za unajimu zinazodaiwa na wanajimu katika kutambua matukio ambayo hayajatokea, na mara nyingine hutokea baadae, mfano: kutoa kwao habari ya nyakati za kuvuma upepo, kuja kwa mvua, kutokea theluji, kuwepo joto na baridi, na kubadilika gharama za bidhaa na mfano wake. Na wanadai kuwa wanadiriki kufahamu hayo kwa

[1] Sahihu Muslim, Hadithi na. 125

utembeaji wa nyota, kukusanyika kwake, na kutawanyika. Na hii ni katika elimu aliyojipwekesha Allah kwayo, haijui elimu hiyo yeyote kinyume na yeye.[1]

Kwa ufupisho kila elimu ya utumiaji wa nyota inayoonesha kuwa nyota inataathira katika mustaqbali wa mambo yaliyofichikana kama kujua kuwa wanandoa watafanikiwa au la, basi hilo halifai, na huitwa elimu hiyo, elimu ya kuathiri (Ilmut-taathiir), ama kutumia nyota kujua muelekeo wakati safari au qibla, hili halina shida, na huitwa elimu hiyo elimu kuwepesishia (Ilmut-taysiir). Hivyo wachumba wazinduke katika jambo hilo, badala yake waswali Swala ya Istikhara kama tutakavyoifafanua kwa kina in shaa llah

6. Wachumba kukaa faragha na kuongea, au mmoja kumshika mwingine, au kubusiana na hatari zaidi kufikia katika kuzini – Tunamuomba Allah stara. Jambo hili wametahiniwa kwalo vijana wengi walioathirika na fikra za kimagharibi hasa hasa wanafunzi wa vyuo vya kati na vyuo vikuu vya elimu ya "secular', wakiona ni jambo la kawaida kufanya hivyo. Na hatari zaidi ni pale ambapo, wanaharakati wa kiislam kujuzisha hilo kwa madai kuwa; watu wawe na malengo ya kuchagua wake bora. Wakaweka kitu kinachoitwa '**Nusra!**'. Wakavunja taratibu za Uislam za kuendea jambo la uchumba, ikawa mtu hatambuliki kwao na binti, bali wao ndio wamekubaliana wawili pekee. Vilevile kuigia katika makatazo ya kufanya mambo kwa faragha kamavile: kukaa faragha, kuongea kwa simu faragha n.k.

عَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ، عَنِ النَّبِيِّ صلى الله عليه وسلم قَالَ :لَا يَخْلُوَنَّ رَجُلٌ بِامْرَأَةٍ إِلَّا مَعَ ذِي مَحْرَمٍ

Kutoka Kwa Ibnu Abbas, kutoka kwa Nabii – Sala n Salamu zimfikie amesema: Asikae faragha mwanaume na mwanamke, isipokuwa (mwanamke) awe na maharimu wake[2]

عن مَعْقِل بْن يَسَارٍ يَقُولُ: قَالَ رَسُولُ اللهِ صلى الله عليه وسلم: «لَأَنْ يُطْعَنَ فِي رَأْسِ أَحَدِكُمْ بِمِخْيَطٍ مِنْ حَدِيدٍ خَيْرٌ لَهُ مِنْ أَنْ يَمَسَّ امْرَأَةً لَا تَحِلُّ لَهُ»

Kutoka kwa Maa'qil bin Yasaar amesema: Amesema Mjumbe wa Allah –Juu yake Sala na Salamu "Kuchomwa mtu kwa sindano ya chuma katika kichwa chake ni bora kwake kuliko kumgusa mwanamke asiye halali kwake[3]

7. Wachumba kutotumia vigezo vya kisheria katika kuchagua mwenza na kuangalia zaidi maslahi ya kidunia, jambo ambalo linapelekea madhara makubwa mno. Kamavile; kutopatikana malezi bora kwa watoto, wanandoa kufanyiana madhara au kupelekea kuuwana kabisa n.k.

[1] A'unul- Maa'buud Juzuu 10 Uk. 285
[2] Sahihul-Bukhaary, Hadithi na. 4935
[3] Swahihut-targhiib wa At-tarhiib, Hadithi na. 1910

SWALA YA ISTIKHARA

Anasema Sheikh A'bdul-Aziz ibn Baaz – Allah amrehemu:

الاستخارة تشرع عندما يهم الإنسان بشيء عنده فيه تردد، يهم بالزواج، يهم بالسفر، يهم بالتجارة في أشياء معينة ويتردد، فهذا يستخير الله، يصلي ركعتين كما أمره النبي صلى الله عليه وسلم، ثم يدعو ربه، يرفع يديه

Istikhara imewekwa katika sheria pale ambapo mtu anakusudia jambo alilo na shaka nalo. Anakusudia kuoa, anakusudia kusafiri, anakusudia biashara katika jambo maalum na anashaka ndani yake. Basi huyu afanye istikhara. Anaswali rakaa mbili, kama alivyoamrisha Nabii –juu yake Sala na Salamu, kisha anamuomba Mola wake Mlezi, ananyanyua mikono yake.[1]

Ama dua anayotakiwa kuomba, ambayo imekuja katika hadithi ni:

اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْتَخِيرُكَ بِعِلْمِكَ، وَأَسْتَقْدِرُكَ بِقُدْرَتِكَ، وَأَسْأَلُكَ مِنْ فَضْلِكَ الْعَظِيمِ، فَإِنَّكَ تَقْدِرُ وَلَا أَقْدِرُ، وَتَعْلَمُ وَلَا أَعْلَمُ، وَأَنْتَ عَلَّامُ الْغُيُوبِ. اللَّهُمَّ إِنْ كُنْتَ تَعْلَمُ أَنَّ هَذَا الْأَمْرَ خَيْرٌ لِي، فِي دِينِي وَمَعَاشِي وَعَاقِبَةِ أَمْرِي فَاقْدُرْهُ لِي وَيَسِّرْهُ لِي، ثُمَّ بَارِكْ لِي فِيهِ، وَإِنْ كُنْتَ تَعْلَمُ أَنَّ هَذَا الْأَمْرَ شَرٌّ لِي، فِي دِينِي وَمَعَاشِي وَعَاقِبَةِ أَمْرِي، فَاصْرِفْهُ عَنِّي وَاصْرِفْنِي عَنْهُ، وَاقْدُرْ لِي الْخَيْرَ حَيْثُ كَانَ، ثُمَّ أرضني به

Ewe Allah! Hakika ninakutaka ushauri kwa elimu yako, na ninakutaka kuweza kwa uwezo wako, na ninakuomba katika fadhila zako tukufu, hakika wewe ni muweza nami sina uwezo, na unajua nami sijui, nawe ni mjuzi wa yaliyofichikana. Ewe Allah! Ukiwa wajua jambo hili – utataja haja yako- ni bora kwangu katika dini yangu na maisha yangu na mwisho wa jambo langu, niwezeshe kwalo, na niwepesishie, kisha nibariki katika jambo hilo. Na ukiwa wajua jambo hili – utataja haja yako- ni shari kwangu katika dini yangu na maisha yangu na mwisho wa jambo langu, basi niondoshee hilo jambo, na liepushe nami, na niwezeshe bora popote lilipo, kisha nifanye kuliridhia.[2]

Na mtu anaweza kuomba dua ya istikhara kama ilivyopokelewa, na hilo ndilo bora, na ikiwa ameshindwa, basi aombe kadri awezavyo hata kwa lugha yake. Anasema Sheikh Ibnu Baaz –Allah amrehemu:

إذا كان ما يعرف هذا الدعاء يدعو بما عنده، يقول: اللهم إن كانت هذه الحاجة فيها خير لي، فيها مصلحة لي، فيسرها لي، وإن كان غير ذلك فاصرفه عني واصرفني عنه. المقصود يدعو بهذا المعنى بالدعاء الذي يعرف، والمعنى الذي يعرف ولا بأس، هذا مسنون مشروع بعدما يسلم من الركعتين، وإن دعا من دون صلاة أو دعا بعد صلاة النافلة المعتادة بعد سنة الظهر أو سنة المغرب أو سنة العشاء أو غير ذلك لا بأس، أو دعا وهو جالس دعاء عاديا يسأل ربه لا بأس.

Pindi itakapokuwa hajui dua hii, aombe kwa alichonacho. Aseme: ewe Allah! Ikiwa haja hii ndani yake ina kheri kwangu, kuna maslahi ndani yake, basi niwepesishie. Na ikiwa kinyume na hivyo, niondoshee jambo hilo, na niondoshe katika hilo jambo. Makusudio ni aombe kwa maana kwa dua aijuayo, kwa maana ambayo

[1] Fataawa Nuuru A'lad-darb, Juzuu 11 Uk 62

[2] Sahihul-Bukhaary, Hadithi na. 1109

anaijua na hakuna ubaya. Dua hili ni sunna na sheria baada ya kutoa salamu ya swala ya rakaa mbili. Na endapo akiomba pasi na kuswali, au akiomba baada ya kuswali sunna aliyozoea kuswali, ima baada ya sunna ya adhuhuri, au sunna ya maghrib, au sunna ya ishaa, au kinyume na hizo, basi hakuna ubaya, au akiomba dua akiwa amekaa kawaida, anamuomba Mola wake Mlezi basi hakuna ubaya.[1]

Mtu akishaswali na kuomba dua, pia anasauriwa aombe ushauri kwa watu wanaomjua huyo binti, mpaka moyo wake utakapotulizana kuingia katika ndoa akiwa anarejea kuikariri istikhara. Ikiwa moyo wake utakuwa mzito au jambo likawa gumu basi aachane nalo, na wala asitegemee kuota ndoto. Amesema Sheikh Ibnu Baaz –Allah amrehemu:

ثم بعد هذا إذا تيسر أن يستشير من يعلم أنه أهل نصح ومحبة له وأهل خبرة يستشيرهم بعد الاستخارة، فإذا مال قلبه إلى أحد الأمرين أخذ بذلك، وإن بقي التردد أعاد الاستخارة وأعاد المشاورة حتى يطمئن قلبه إلى أحد الأمرين.

Kisha baada ya hili (dua na swala ya istikhara), ikipatikana wepesi wa kuomba ushauri kutoka kwa anayemjua ni katika watu wenye kutoa nasaha na mapenzi na katika watu wa kheri, atawaomba ushauri baada ya Istikhara. Itakapokua moyo wake umeelekea katika moja ya mambo mawili atachukua hilo moja, na ikiwa imebaki shaka, atarejea Istikhara na atarejea kutaka ushauri mpaka moyo wake utulizane katika moja ya mambo mawili.[2]

HITIMISHO

Mpaka hapa tutakuwa tumekalisha masala yanayofungamana na uchumba, na Makala na. 3 tutatazamia mambo yanayofungamana na kifungo cha ndoa kwaa idhini yake Allah.

[1] Fataawa Nuuru A'lad-darb, Juzuu 11 Uk 62 - 63
[2] Fataawa Nuuru A'lad-darb, Juzuu 11 Uk 77

MAREJEO

- **Vitabu va dini**

Abdul-A’ziz Ibn Baaz. (1441 H). *Fataawa Nuuru A’lad-darb*. Riaasatu Idaaratil Buhuuth Al-I’lmiyyah Wal-Iftaai

Abuu Daud. (1323 H). *Sunanu Abii Daud*. Al-Matw-baa’h Al-answaariyyah

Abuu I’sa At-tirmidhy. (1997 M). *Sunanu At-tirmidhy*. Daarul-gharbil-Islaamiyyah

Ahmad ibn Hanbali. (1416 H). *Musnadul Imaam Ahmad ibn Hanbali*. Daarul hadith

Al-a’dhwiim Aabaad (1415 H). *A’unul Maa’buud*. Daarul-kutub Al-I’lmiyyah

Albukhary. (1414 H). *Sahiihul Bukhary*. Daaru ibn Kathiir

Al-lajnatu Addaaimah lil-buhuuth Al-Ilmiyyah. *Fataawa Al-lajnat Ad-daaimah – Al-mujuua’h Al-uulaa*. Riaasatu Idaaratil Buhuuth Al-I’lmiyyah Wal-Iftaai

Al-Mardaawiy (1415 H). *Al-Inswaafu fii Maa’rifatir-raajih Minal-Khilaaf*. Hajru lil-twibaa’h

Ibnu Faaris (1431 H). *Muu’jamu Maqaayiisil-lughah*. Maktabatul-Mustwafah

Ibnu Qudaamah. (1414 H). *Al-kaafiy fil-fiqhil-Imaam Ahmad*. Daarul-qutbil-Islaamiyyah

Ibnu Uthaymiin. (1433 H). *Ash-sharhul-mumtii’*. Daarul-Ummah

Muslim ibn Al-hajjaaj. (1374 H). *Sahihu Muslim*. Matba’tu I’isa Alhalaby

Naaswirud diin Al-albaaniy . (1431). *Aadabu Az-zifaaf*. Maktabatul-Maa’rif

Naaswirud diin Al-albaaniy. (1421 H). *Sahiihu Attarqhiib wa Attarhiib*. Maktabatul Maarif

- **Vitabu na majarida yasiyo ya dini**

Talbot, Angela. (1960). *Woman*. Future PLC

BAKITA. (2015). *Kamusi Kuu ya Kiswahili*. Longhorn Publisher PLC

Imekusanywa usiku wa Jumaanne, 11 Dhul-qii’dah 1447 = 27/04/2026

Zanzibar, Tanzania

+255 772 808 543/ +255 714 036 096